Dozia no. 53



Mabinti wawili wakirejea majumbani wakitoka kuteka maji katika kijito ambacho jumuiya ya wakaazi waishio mashambani huchangia na wanyama mwitu, 29 July 2020.

Sifa: New Frame / Magnificent Mndebele

# *Utangulizi*

Kukulia katika shamba huko Nyarha,jimbo la Eastern Cape nchini Afrika Kusini,nilipia utoto mzuri. La awali ilikuwa ile hali ya kutokuwa na hatia ya utoto,vile kuwa binti mdogo nikikimbia kwa uhuru na kucheza na *oonopopi ('wanasesere'), iriyasi*('kukimbia'), *undize*('kombolela'),*upuca* ('soro')na *ugqapsi* ('kuruka kamba'). Ile hali ya u-jamii,uhuru na kutegemeana kijamii ilikuwa furaha yangu nyingine. Wazazi wangu waliweza kunipeleka katika nyumba za majirani pasi kuhofu juu ya usalama wangu. Mama yangu mara nyingi alinituma katika majumba ya majirani kuomba *igaqa le beef stock('pande la nyama ya ng'ombe')* ili tujipatie mlo kama hakuwa na kitu, ama *intwana ye swekile('sukari')* kama ilimwishia.

Muda pekee niliokuwa niliohisi kutoweka kwa uhuru ule na hali ya kuwa na chochote kuyoyoma ni nilipomuona mzungu aliyekuwa mmiliki wa shamba. Punde ningejisikia kukumbwa na hofu kubwa. Hofu ile ilikuwa ya namna zote yaani kujifunza na kufunzwa; tulifunzwa kuwa hofu ilikuwa ni aina ya heshima.Wakati tukipokea maelekezo kutoka kwa mkulima(mzungu) babu yangu alikuwa tofauti, akiinamisha kichwa chake na kukwepesha macho.

Baba yangu alipokuwa akisikia muungurumo wa sauti ya pikipiki ya mkulima ukikaribia alificha haraka bia aliyokuwa akiinywa.

Aina ya mahusiano niliyoielewa baina ya mmiliki wa shamba na wafanyakazi na wakaazi wa shambani ni sehemu ya muundo wa kijamii katika shamba.Mashamba si tu maeneo ya uzalishaji; yameundwa katika hoja ya 'ubwana'-utaratibu unaoongoza mahusiano ya kimamlaka katika kina cha utambulisho wa kijamii na maisha ya kila siku. **[2]** Kama aina ya udhibiti na kuonesha mamlaka/nguvu yake, mmiliki wa shamba wa kizungu alihitaji uoneshe kama unamuogopa. Kuonekana humuogopi ilitiizamwa kama utovu wa heshima hususani kama ulikuwa na utayari wa kuhoji chochote ambacho mmiliki wa shamba alikisema ama kukifanya. Kama mtoto, niliona ni jambo la kustaajabisha sana baba alipokuwa akiniambia kuwa eneo lote kubwa la eNyarha lilikuwa lilikuwa miliki ya mzungu. Hakuna mtu mweusi hata mmoja aliyekuwa  na ardhi yeyote. Kama mtu mzima, nilikasirishwa nilipofahamu kuwa vizazi vitano vya familia yangu wameitumikia familia hiyohiyo moja, lakini hatukuwa na dai wala sauti ya aina yeyote katika ardhi ile. Nilihoji kwanini nguvu kazi ya famila yangu  waliyoitoa kwa miongo mingi ilizaa matunda  kwaajili ya wamiliki wa wa ardhi wa kizungu na vizazi vyao pekee. Sikuweza kuridhia habari ya vizazi vitano na kazi ngumu na maisha tuliyokuwa tukiishi: maisha ya ufukara.

Mahusiano ya nguvu kazi katika mashamba ya Afrika Kusini bado yanazidi kushikiliasuala la rangi,jinsia na matabaka kama tabia ya msingi ya kazi  na maisha. Wakulima wa mashamba makubwa ya kibiashara, kama walivyo mabepari wengine wote wanaendeleza mzunguko wa utumwa ambao unazaa umasikini wa kizazi hata kizazi kwa wafanyakazi wao na wanajihusisha na matendo  ya unyonyaji nguvu kazi mfano kuwafanyisha kazi kwa saa nyingi na kuwalipa ujira wa kitumwa(finyu).

Kadiri wanavyotumia muda wao mwingi kufanya kazi, ni adimu kwa wafanyakazi kupata  muda wa kutosha kwaajili ya kuimarisha mwili, ama kutumia akili kufanya shughuli nyingine, kufanya shughuli za burudani ama kusafiri mbali kutoka katika mashamba yao. Ardhi na wafanyakazi vyote ni vitovu vya unyonyaji. Wafanyakazi wa mashambani walipwa malipo duni kuanzia Randi 2000 hadi 6000(sawa na dola za marekani 136-408) kwa mwezi. Kima chao kidogo cha mapato hakitoshi kuwakimu wao wenyewe,jambo linalowalazimisha kuishi katika hali ya chini ya kujikimu, na mara nyingi hulalamika ya kuwa  hawamudu kununua chakula ama kulipa gharama za shule kwa watoto wao.

Wafanyakazi wengi wa mashambani pia  wanataaluma wameonesha juu ya uwepo ya wa kutolipwa, kutothaminiwa, na  nguvu kazi isiyoonekana mara nyingi  ya  uzazi na ulezi(kuendeleza maisha), mfano kujifungua, kuiweka nyumba sawia, kuuguza wagonjwa, upishi,usafi, na kadhalika. Nguvu-kazi hii ipo katika msingi wa mfumo wetu wa uchumi, kwa kuwa si

tu inazalisha viumbe na jamii bali inawapa tabaka la mabepari hakika ya kupata wafanyakazi. Kwa maneno ya Susan Ferguson:

> …uelewa wetu kuhusu ubepari haujatimu ikiwa tunautizama tu kama mfumo wa kiuchumi unaohususha wafanyakazi na wamiliki wa njia za uzalishaji mali  na tukashindwa kubainisha kwa upana uzazi-jamii(social reproduction) wa mfumo-ambao ni,nguvu kazi ya uzazi ya kila siku na vizazi kwa vizazi inayotokea majumbani,shuleni,hospitalini,magerezani na kadhalika -ambako kunadumisha msukumo wa ulimbikizaji.**[3]**

Kwa muktadha wa mashambani, ujira kiduchu wa wafanyakazi unakwaza suala  la uzazi wa  kijamii kwa  familia zao.Katika mfumo huu, ambao wafanyakazi wa mashambani wanafungamanishwa na ardhi pasipokuwapo umiliki kwayo kwa vizazi kadhaa, ajira yao inasadifu kila kitu katika ulimwengu wao: kuifanyia kazi ardhi,kuishi katika ardhi kuiboresha na kuiendeleza ardhi, kuleawawatotot katika ardhi, kuzika wanafamilia na wapendwa wao katika ardhi, kuwa na mafungamano  ya aina yeyote na ardhi,kuipenda ardhi, na kuiita ardhi maskani, lakini kamwe kutoimiliki ardhi.

Bab'Kubheka, mfanyakazi wa shamba mstaafu mwenye umri wa miaka 71 na mkaazi wa Newcastle, KwaZulu-Natal, anafafanua namna tabaka la kijamii la wazazi wake  limeathiri maisha yake na ya umbu zake. Anasema:

Tulipokwa uwezo na mfumo. Baba zetu walikuwa wapangaji ardhi ambao hawakuwa na fedha za kutusomesha.**[4]**Walipangiwa pia na idadi ya ng'ombe walioruhusiwa kufuga na wapi pa kuwaweka**.** Hawakupata malipo ya aina yeyote, hivyo wanafahamika kama wapangaji ardhi… tulishindwa kupata elimu katika ngazi ya kati ama juu kwa kuwa wazazi wetu hawakuwa na fedha.Tuliishi kwa chakula walichokizalisha.Hatukuwa tukiuza chochote.Waliamka na kwenda kufanya kazi kwa wazungu bila malipo ya aina yeyote.Hivi sasa tunalo tatizo ambapo watu wetu-watu weusi-hata sasa hawana ardhi.**[5]**

Kisa mkasa cha Bab'Kubheka's kinashadaia kwa mfano alichodai Walter Rodney's kuwa 'kupoteza wakati au kujongea taratibu wakati wengine wakipiga hatua kubwa kuelekea mbele ni sawasawa na kwenda nyuma'.**[6]** Ufukara una hama na kujizalisha to kizazi kimoja hata kingine.**[7]**



Juu  ya kazi za shamba , wanawake kama Nozibonelo Mavis Dayi wanawajibika kwa kiasi kikubwa kwenye suala la uzazi na malezi ya jamii katika mtindo wa kazi ya ulezi isiyo na malipo katika kaya, 21 Machi 2021.

Sifa: New Frame / Bonile Bam

## *Kuhusu Dozia Hili*

Huku ikiondoka katika dhahania zilizounda mtizamo kuwa suala la ardhi ni suala la kitaifa la wachache nchini Afika Kusini, dozia hii inajikita  juu ya wafanyakazi wa mashambani na kama wachangiaji muhimu kwenye mjadala kuhusu ardhi. Inaibua hoja mbili. Ya kwanza ni kuwa sababu kuu

ya umasikini wa vizazi na vizazi wa wafanyakazi wa mashambani weusi ni unyonyaji wa nguvu kazi yao. Shamba, kama zilivyo juhudi nyingine za kibepari, inategemea kushushwa thamani kwa nguvu-kazi ya watu weusi.

Wamiliki wa mashamba wanaitumia nguvu-kazi ya watu weusi kama ya isiyo na thamani na kuendelea kushikilia aina fulani ya ukabaila ambapo wafanyakazi wasio na ardhi wanafungamanishwa na ardhi ya mmiliki na wanalazimishwa kuwa watiifu. Matishio ya kupoteza kazi na kuondolewa kwenye mashamba ni njia ambazo wamiliki wa mashamba wanazitumia kuvuna utiifu,jambo ambalo lina madhara kwa wafanyakazi wa mashambani: kuhoji chochote ni kuhatarisha vyote.

Pili, doza hii inaibua hoja kuwa wale wenye kuifanyia kazi ardhi wanastahili kuwa wanufaishaji wa kwanza, kinyume chake, wamekuwa wakitengwa na faida na ustawi wa kumiliki ardhi kwa vizazi na vizazi. Pia wametengenezwa kwa kiasi kikubwa kutoonekana katika takwimu za kazi na kutengwa katika mijadala ya ardhi na ni mijadala ya kitaifa ya sera za mgawanyo wa ardhi. Kuuelewa mtizamo wao ni muhimu kwaajili ya kuendeleaza programu ya mageuzi ya ardhi itakayowanufaisha wale wenye kuifanyia kazi ardhi, hii ndio sababu dozia hii inauleta mchango wao katika mjadala kuhusu ardhi, na ndio sababu Tricontinental: Institute for Social Research ilifanya mahojiano na wafanyakazi wa mashambani kutoka majimbo ya Afrika Kusini ya Eastern Cape, KwaZulu-Natal, Northern Cape, and Western Cape kwaajili ya dozia hii.

Suala la ardhi nchini Afrika Kusini lina pande nyingi ikiwamo,mchango wa mashamba yanayomilikiwa na wazungu,mamlaka za kijadi za tawala za zamani za 'Bantustani', na suala la ardhi ya mijini.Dozia hii imejikita katika ka kwanza.



Wafanyakazi wa mashambani wanawake wanakabiliwa kwa ziada na kutokuwepo usawa katika mgawanyo wa ardhi na mazingira ya kazi.Wafanyakazi wa zamani Freeda Mkhabela,Lucia Foster,and Gugu Ngubane(kutoka kushoto kwenda kulia) ni miongoni mwa wanaharakati wanaopambana na changamoto ya kutokupatikana kwa ardhi sambamba

na ujira finyu na mazingira magumu ya kazi na kuhesabu kwa wafanyakazi wa mashambani, 26 Mei 2021.

Sifa: New Frame / Mlungisi Mbele

## *Historia yetu imekuwa wakati wetu wa sasa*

*'Wakati haupiti wala kusonga;unajilimbikiza, hata katika kusahau ama kutamatisha,hata katika kazi nzito inalazimu kusalimu amri juu ya yaliyokuwa,ama kufidia kwayo,ama kushughulikia matokeo yake mabaya'.***[8]**

*– Ian Baucom*

Akiandika juu ya kadhia ya wafanyakazi wa mashambani nchini Afrika Kusini mwaka 1990, mwanahistoria Wendy Davies alionesha namna gani mtu anavyoweza anaweza kufuatilia mgawanyo wa ardhi kwa kutizama tu mstari wa rangi ya ngozi za miili ya watu na pia kushushwa thamani kwa nguvu kazi ya watu weusi kupitia historia**[9]** pamoja na kushushwa thamani kwa nguvu-kazi ya watu weusi kihistoria. Davies allifafanua kwa kina namna wafugaji weusi na jamii za wakulima walivyoporwa ardhi na wimbi la walowezi wa kizungu katikati ya karne ya kumi na saba na kuendelea. Walowezi wa kizungu walijipatia 'umiliki' wa milki mpya kwa kushinda

vita dhidi ya falme na milki za watu weusi.Kupitia mchakato wa kuandika mikataba ya kishenzi(bogus treaties) na hati miliki za kuuza, walihakikisha masharti ni ya kuwanufaisha wao kwa kiasi kikubwa.Ingawa kulikuwa na upinzani mkubwa kwao, matumizi ya vurugu ya walowezi wa kizungu yaliwezesha mafanikio ya uporajina ukaliaji wa ardhi walizozipoka.

Walowezi Waingereza na Wadachi('Makaburu') katika Afrika Kusini walihitaji nguvu-kazi kwaajili ya mashamba, mashamba makubwa , na migodi katika ardhi walioipora kutoka kwa watu weusi wa Afrika Kusini.**[10]** katika maneno ya Davies, wakulima wa wazungu walisisitiza kuwa 'uwepo wa watu weusi utavumiliwa ikiwa tu watawafanyia kazi wazungu'.**[11]** Beberu la wa kiingereza Cecil John Rhodes iliweka wazi mtizamo huu katika hotuba yake mwaka 1894 katika bunge la la Cape, alisema 'ifikishiwe habari hii majumbani[kwa watu weusi] kwamba kwa siku zijazo,tisa katika kumi kati yao watatakiwa watumie muda wote wa maisha yao katika kazi za kila siku,kazi zisizo za mashini na kazi ngumu'.**[12]** Mchakato huu ulitekelezwa kwa kuwalazimisha watu weusi kuwafanyia kazi wakulima wazungu kwa kunyang'anya ardhi zao, kuangamiza nyezo zao za kuishi na kuanzisha kodi ili kuwalazimisha kwenye aina ya uchumi wa kuuza nguvu kazi.**[13]**

Davies anafafanua kwamba, 'wakulima wazungu walipofanikiwa kudhibiti ardhi takribani yote, wakulima weusi walianza kuingia katika kilimo cha

kushirikiana/pamoja na “wamiliki” wao wazungu. **[14]** Kilimo cha pamoja ilimaanisha kuwa  wale waliofanya uzalishaji katika ardhi husika  walitoa sehemu ya mavuno yao (mara nyingi asilimia 50) kwa ‘mmiliki’ ili kupata haki ya kuitumia ardhi tena. **[15]** Mashamba yalikuwa na bado ni maskani kwa wafanyakazi wa kupanga/kukodi, kundi jingine ambalo linatoa nguvu-kazi isiyo na malipo  kwa wamiliki wa mashamba ili kupata haki ya kutumia ardhi, kwa kufanya kazi bila malipo katika miezi sita katika mwaka. Kuna wakaazi wa mashambani weusi ambao wanaishi na familia zao katika mashamba wanayoyamiliki, wachache miongoni mwao wameajiriwa kwa kazi za mashambani kwa muda mfupi ama ajira za kudumu.**[16]**

Mchakato huu wa ulimbikizaji kwa uporaji una madhara makubwa kijamii na kitabaka katika bara la Afrika. Kama Issa G. Shivji afafanuavyo, ‘utofauti tunaouona baina ya  wafanyakazi na wamiliki,baina ya  maeneo ya mijini na vijijini’  na baina ya nchi zilizotawaliwa na zili za metropoli ni ni matokeo ya mbadilishano usio sawa unaokwenda karne nyingi nyuma’. **[17]**



Mzee na mkaazi wa shamba mstaafu na mfanyakazi wa mashambani anaibeba kumbukumbu ya wazee wake kwa masimulizi ya historia.Nomabhaso Skenjana anaonesha eneo ambalo makaburi ya familia yake yapo tangu miakaya 1880 mpaka yalipoharibiwa kipindi cha Apartheid(zama za sheria za ubaguzi wa rangi),shamba lilipopokwa na wazungu,4 Agosti 2021.

Sifa: New Frame / Bonile Bam

# *Mgawanyo wa Ardhi kwa Jinsia na Jamii za Watu Kwa Minajiri ya Rangi ya Ngozi*

# *Umhlaba wookhokho Bethu! Ardhi ya Wazee Wetu!*

'Asili haizalishi mali- watoa nguvu kazi upande mmoja na wamiliki wa mali upande wa pili'.***[24]***

– *Issa G. Shivji*

Wafanyakazi wa mashambani wanahusiana na ardhi kwa mguso wa umiliki na urithi wa utamaduni, mara nyingi wakiichukulia kama *umhlaba wookhokho bethu* ('*arhi ya wazee wetu*'). Kauli hii ina maana nyingi kwa muktadha wa jamii za wakulima.Si tu kwamba wanafikiri juu ya ardhi wazee wao kwa lensi ya kihistoria; pia wanalichukulia hili kama suala ambalo halijatatuliwa kuhusu uminywaji haki, wakilielewa kuwa lina mizizi ya kihistoria na unyonyaji kwa vizazi vingi uliofanywa na wamiliki wa mashamba wa kizungu-jambo linaloendelea mpaka leo.Wafanyakazi wa mashambani wanaitizama ardhi kama iliyoibiwa kutoka kwa wazee wao waliowatangulia kupitia mchakato wa uporaji wa ukoloni na ulaghai ulioboresha maendeleo ya ubepari. Katika maelezo yao, hii si tu ilipelekea kupoteza ardhi na mifugo lakini pia iliharibu

dhana ya mahusiano ya ardhi na dhana ya matumizi ya ardhi iliyokuwepo kabla ya ukoloni.Uelewa kuwa ardhi ni kwaajili ya ustawi wa wote-kwamba inaweza kutumiwa na wote-iliharibiwa vibaya.

Kama tujuavyo kuwa ulimbikizaji-asili ulikuwa kiungo muhimu mno kwa utawala wa kikoloni barani Afrika.Wafanyakazi wa mashambani ni wakosoaji wakubwa wa umiliki haramu wa ardhi wa wazungu wachache na wanatoa hoja  kuwa huo ndio mzizi wa ubaguzi wa rangi.Katika mataifa ambayo yamepitia ukoloni wa kilowezi, Shivji anafafanua namna ambayo ardhi kubwa zilitengwa na wenyeji wake na namna ambazo nchi hizi zilipitia mchakato wa awali wa uporaji ardhi. **[25]** Anaelezea kuwa huu ni ‘ulimbikizaji-asili katika ubora wake’, mchakato halisi ambao hali ya ya ulimbikizaji wa ubepari ulizaliwa.**[26]** Mchakato huu ndio ulizalisha ‘ziada ya watu’ wasiokuwa na ardhi ambao hawakuwa na haki rasmi ama zakimila, hali iliyopelekea kuzaliwa kwa tabaka la wafanyakazi wa viwandani toka kwenye sehemu kubwa ya watu wetu. Hii ilizalishakundi la watu ambao hawakuwa na  shughuli ya kufanya kwaajili ya kujikimu na kuzalisha tena isipokuwa kwa kuuza nguvu kazi yao.

Baada ya kipindi kirefu cha muda,umilikaji wa ardhi ya kilimo umegeuka kuwa ni suala la rangi ya ngozi ya mwili. Kupata ardhi nimchakato wenye gharama kubwa  ambao ni wenye kumudu wameendelea kuwa wazungu wachache ambao wamelimbikiza rasilimali na utajiri wa kumudu kununua ardhi kwa vizazi vingi. Utajiri ambao wakulima wanaupata

kutoka katika ardhi unawawezesha kupata ardhi zaidi na zaidi na kuwekeza zaidi juu ya mali walizokuwa nazo. Wafanyakazi wa mashambani kwa upande mwingine si sehemu ya umiliki wa mali hii. Wanawazalishia mali wamiliki wa mashamba wa kizungu ilhali wao wakiendelea kufubaa, watoto wao wanarithi umasikini wa wazazi wao. Hivi ndivyo namna pengo la utajiri linavyokita mizizi zaidi, kama inavyojionesha kwa hoja ya kuwa asilimia 1 ya matajiri wa Afrika Kusini wanaomiliki kibinafsi angalau asilimia 40.8 ya utajiri wote wa nchi ilhali asilimia 90 ya walioko chini kiutajiri wakimiliki asilimia 20.1.**[27]**

Kutokea katika mchakato wa kihistoria wa uporaji mkali, umiliki wa ardhi na utajirisho wake una maana ya moja kwa moja juu ya mahusiano ya nguvu/mamlaka ambayo wamiliki wa mashamba wanaendelea kuwa na haki zaidi kushinda wafanyakazi ambao wanawadhibiti. Kama Carmen Louw wa mradi wa ufeminia wa 'Women on Farms Project' anavyofafanua, 'Mashamba katika Western Cape yapo tangu zama za ukoloni na,kwa hiyo, wanayo haki kwa mgawanyo wa ardhi'. **[28]** Ni wazi kuwa wafanyakazi wa mashambani hawatizami uporwaji wa kihistoria kuwa ni jambo lisilohusiana na mapambano yao ya sasa ya ardhi na nguvu kazi.**[29]**

Hili ni jambo moja la msingi kabisa,wafanyakazi wa mashambani wanahitaji kupata makaazi yao wenyewe ili kuboresha maisha yao, familia zao na vizazi vijavyo.Oom Boetman,mfanyakazi wa mashambani

aliyebobea katika uundaji wa uzio katika mashamba huko Colesberg, Northern Cape, anafafanua: *'Ons soek beter bly plek, dan sal ons ook beter lewe'* ('Tunataka makaazi bora ili sisi nasi tuweze kuishi maisha bora'). **[30]** Vivyo hivyo, Tanie Leana, mkaazi wa mashambani katika jimbo hilohilo ambaye ana watoto sita na mjukuu mmoja wa kiume, anatamani serikali ingeendeleza jamii yao. '*Ons soek net huise*' ('tunahitaji nyumba tu'), na binti yake anasema.**[31]**



Ufugaji, *ukulima* ('kulima mazao'), na *ukufuya* ('kufuga') ni vyanzo vya maisha kwa wafanyakazi wa mashambani kama Ephraim Muggibelo Simelane, 30 Julai 2020.

Sifa: New Frame / Magnificent Mndebele

# *Nguvu-kazi ya kizazi hadi  kizazi*

*'Hatuwezi kushughilika na suala la utu wa wafanyakazi wa mashambani kama hatutopata ardhi.*

*Suala la ardhi halina mjadala!'*

*– Trevor Christians, katibu mkuu wa Commercial, Stevedoring, Agricultural, and Allied Workers' Union (CSAAWU)*

Ingwa mkataba wa uhuru(Freedom Charter) unaahidi kuwa 'ardhi itagawiwa kwa wale wanaoitendea kazi', na kifungu 25(5) cha katiba ya Afrika Kusini kinaahidi haki sawa kwa matumizi ya ardhi,ahadi hizi bado hazijatekelezwa. Vizazi kadhaa vya familia wafanyakazi wa mashambani wasiokuwa na ardhi wametumia nguvu kazi yao katika uzalishaji na utunzaji wa mashamba maeneo mbalimbali nchini.Katika mchakato,wamechangia kwa kiasi kikubwa kuzalisha utajiri  wa wamiliki wa mashamba. Wafanyakazi wa mashambani  wanaunganisha mchakato huu na mapambano ya wafanyakazi ya wazee wao waliowatangulia; nguvu-kazi ya vizazi ya muda mrefu mashambani ni lazima ichukuliwe

kuwa ni sababu muhimu si tu kuhalalisha haki ya wafanyakazi wa mashambani', bali pia kudai umiliki wa ardhi.

Wafanyakazi wa mashambani Baw'uSukwini na Baw'uMkwayi wote wanagusia hoja hii.Mfanyakazi wa mashambani wa kizazi cha tano, Baw'uSukwini, anazungumza juu ya kisa cha familia yake katika shamba la mifugo huko,jimbo la Eastern Cape:

Nadhani baba yangu ni wa kizazi cha nne katika shamba lile…Baba yangu alikuwa na miaka zaidi ya 80 alipofariki.

Baba yangu hakuwahi kwenda shule;alizaliwa[shambani]…alikulia pale na kufanya kazi pale.Alizeekea na kufia pale.Umbu wetu wote nane…walikulia katika shamba lile na kufanya kazi katika shamba lile…wafanyakazi wa mashambani ndio wanaoifanyia kazi ardhi ile mpaka wanaota mvi.Kwanini serikali hainunui shamba? Baada ya kununua shamba,wanaweza kwenda katika mashamba kutizama wale wanaoishi kwenye mashamba [yamilikiwayo na wazungu].Serikali inaweza kusema mashamba yamenunuliwa kwaajili yao kuishi ili wasilazimike kuhamia katika katika miji.**[32]**

Baw'uMkwayi, mfanyakazi wa mashambani mstaafu katika shamba jingine la mifugo huko Nyarha, jimbo la Eastern Cape, anasimulia kisa chake :

Wote[familia yangu] walifanya kazi katika shamba… Mimi pia nilifanya kazi pale kwa miaka 20…[na] mke wangu pia alifanya kazi katika shamba lile…kwa miaka 20. Tulipoondoka pale,hakuchukua chochote; aliondoka mikono mitupu.**[33]**

Wafanyakazi wengi wa mashambani hawana mikataba rasmi ya ajira na mafao. Kama Baw'uMkwayi na Baw'uSukwini waelezavyo, ni kawaida kwa wafanyakazi wa mashambani kuishia kutopata pensheni ama namna ya kujikimu uzeeni, hali inayowafanya wawe tegemezi kwa watoto wao.Kwa mtindo huu,wa nguvu-kazi vijana wanafanya kazi katika mashamba kusaidia wategemezi wa rika mbalimbali.

Ryno Filander, rais wa CSAAWU, chama cha wafanyakazi wa mashambani jimbo la Western Cape,anasimulia kuwa,yeye, baba yake, na mama yake wote wanafanya kazi katika shamba la mvinyo huko Langeberg.Anabainisha masuala mawili yaliyopo katika shamba:vizazi vingi vyenye utajiri na mamlaka vya wamiliki mashamba na vizazi vingi vyenye umasikini na udhalili vya wafanyakazi wa mashambani. 'Kama una ardhi, una mamlaka', anasema. Tatizo jingine, Ryno anafafanua, ni '*mfumo wa* dop'. **[34]** Katika mfumo wa dop, waajiri wanawalipa waajiriwa wao mvinyo wa bei ndogo, ama dop.Ingawa mfumo wa dop ulipigwa marufuku Afrika Kusini miaka ya 1960,mwishoni mwa miaka ya 1990 watafiti walikadiria kuwa takribani aslimia 2 mpaka 20 ya mishahara katika jimbo la Western Cape ilikuwa ikitolewa kwa mtindo wa

pombe.**[35]** Ulevi umeendelea kusalia kuwa moja kati ya changamoto kubwa za afya ya jamii nchini Afrika Kusini-hususani katika jimbo la Western Cape.



Wanachama wa Commercial, Stevedoring, Agricultural, and Allied Workers' Union (CSAAWU) wakiandaman huko Cape Town  kupinga mazingira magumu ya kazi na mazingira magumu mashambani, 21 Septemba 2019.

Sifa: New Frame / Barry Christianson

# *Grave Matters*

Mashamba pia yamekuwa maeneo muhimu kwa masuala ya kiroho kwa wafanyakazi wa mashambani ambao wazee wao walizikwa katika ardhi hiyo.Kwa wafanyakazi wa mashambani, makaburi ya wazee wao ni ushahidi wa kutosha juu ya ukaribu kati ya kazi na maisha ndani ya mashamba. Dhana za maskani na kujihis kuwa na mahala fulani zinashwishiwa na unganiko la kinasaba baina ya walo hai *kunye nezinyanya ('na wazee waliofariki')***.** Hii ni moja ya sababu kuu ya kwanini familia zinaishi mashambani licha ya kuwepo kwa unyonyaji na manyanyaso**.** Kama MaNkomo, mfanyakazi wa mashambani tuliyezungumza naye huko Mto Mooi, KwaZulu-Natal, alivyofafanua, 'Hatutaki kuondoka katika mashamba haya kwa kuwa wazazi wetu na wazazi wa wazazi wetu wamezikwa hapa'.**[36]**

Hasara 'isiyoshikika'-kiungo muhimu kiroho kati ya walio hai na wafu-ni jambo muhimu la kuzingatia kama tutataka kuhakikisha fidia yenye kuhuisha na haki kwa wafanyakazi wa mashambani. Kazi ya Dineo Skosana inachunguza jitihada za kupinga uhamishwaji wa makaburi ya waafrika 1000 kutoka Shamba la Tweefontein huko Ogies,Mpumalanga kwenda eneo jingine, hali inayopelekea vizazi vya walio hai kuripoti hisia zao za 'hali ngumu kiroho na kutenganishwa na wazee wao'. **[37]** Kwa kulichunguza jambo hili, Skosana anaainisha kushindwa kwa malengo ya

baada ya zama za ubaguzi wa rangi kutibu madhila ya ukiukwaji haki ya zamazilizopita. Anajenga hoja kuwa madhaifu katika mfumo wa sheria yamejenga mazingira ya sheria rafiki kwa soko, mfano Sheria ya Madini na Maendeleo ya Rasilimali za Petroli (ya 2002), ili kutangua ulinzi unaotolewa na Sheria ya Rasilimali za Urithi wa Taifa (ya 1999), hali inayopelekea aina mpya za ubaguzi.**[38]**

Kwasasa, utawala wa ardhi hauhusishi kuzingatia utamaduni au historia na unaendelea kuongeza maumivu na kihoro kwa wasiokuwa na ardhi.Hii inachangia kushindwa kunako fedhehesha kwa programu ya mageuzi ya ardhi inayotekelezwa kwa sasa na dola. Wafanyakazi wa mashambani wanaona makaburi ya wazee wao kama ushahidi wa nguvu kazi iliyonyonywa na dai halali la kisiasa-kwamba idadi ile ya watu waliozikwa walikuwa wafanyakazi wa kupangishwa na wafanyakazi wanaonyonywa ambao walihakikisha mashamba  yanastawi. Makaburi haya ni ushuhuda wa wale waliohimili sulubu ya ubepari katika sura ya ubaguzi wa rangi. Bhut'Ben, mfanyakazi wa shamba wa kizazi cha pili huko Mto Mooi, KwaZulu-Natal alizungumzia jambo hili kwa upana zaidi: '*Umphakathi wa-la awukho esimeni esi-right ngokwe nkululeko, kuthiwa sisenkululekweni. Cha as'kabi khona thina. Sisagqilazekile*' ('Jumuiya yetu hapa haijaonja uhuru.Tunaambiwa tuna uhuru lakini hapana,hatujaupata hapa kwetu.Bado tupo utumwani').**[39]**

# *Addressing Food Insecurity*

Ripoti iliyotolewa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa inaonesha kuwa uhaba wa chakula tayari ni janga la kiulimwengu, maana yake ni kuwa 'watu kwa muda wote hawamudu kiuchumi na kijamii kupata chakula salama chenye virutubisho kinachokidhi viwango viwango na vipaumbele vinavyoshauriwa kiafya'. **[40]** Ripoti hii inakadiria kuwa , mwaka 2020, kati ya watu milioni 720 mpaka milioni 811 ulimwengu mzima walikubwa na janga la njaa wakati moja ya tatu ya watu wote duniani (watu bilioni 2.37) walikuwa hawamudu kupata chakula cha kutosha.**[41]**

Licha ya ukweli kuwa wafanyakazi wa mashambani nchini Afrika Kusini-na ulimwenguni kwa jumla-wanaipa(kwa uzalishaji) jamii chakula,wao wamesalia kuwa katika kundi lilio hatarini kukumbwa na uhaba wa chakula.**[42]** Tunachokula, kunywa na kuvaa vyote washukuriwe wafanyakazi wa mashambani. Japokuwa stadi na weledi waoni muhimu kwa uchumi, nguvu kazi yao imeendelea kushushwa thamani.Wafanyakazi wa mashambani wa msimu (mara nyingi wanawake) ambao mara nyingi huajiriwa kwa nusu mwaka mara nyingi hukumbwa na changamoto ya kutokuwa na uhakika wa ajira hasa ukizingatia hawana ardhi zao wenyewe wanazoweza kuzalisha chakula

kwa mwaka mzima. Mabadiliko ya tabia nchi yamepelekea kilimo kuwa fani hatari, hasa kwa watu wa kipato cha chini ulimwenguni.

Moja kati ya hoja zinazoibuliwa kukosoa suala la ugawanywaji-mpya wa ardhi ni dhahania ya hatari kuwa hilo litaathiri kwa uhasi suala la usalama wa chakula. Dhahania hii si tu inapuuzia kuwa mabilioni ya watu ulimwenguni tayari wanakumbwa na janga la uhaba wa chakula, lakini pia inaegemea kwenye uzalishaji wa skeli kubwa na uundaji chini ya ubepari kama njia pekee kuelekea mbele. Kuliko kujali hakika ya usalama wa chakula kwa wote, mashaka ya kibepari yanajikita katika hofu kwamba ugawanywaji-mpya wa ardhi utavuruga mapato ya faida zitokanazo na kilimo cha mashamba makubwa na uzalishaji wa chakula.Wakati wafanyakazi wa mashambani wengi wao wakiwa ni wazee, wanaomba kutambuliwa kwa milki za ardhi kwa wakulima wadogo, ambapo wamiliki ardhi wadogo wanaishi kwa kuzalisha katika ardhi,*ukulima* ('kulima mazao') na *ukufuya* ('kufuga wanyama') na hawakomei katika kukimu familia pekee. **[43]** Kwa ujumla, wafanyakazi wa mashambani wanaikosoa dhahania  kwamba wakulima wa kizungu ndio pekee wenye uwezo wa wa kulima na teknolojia yenye nguvu na ndio wazilishaji hodari pekee, ilhali wakulima weusi wakilima kwaajili ya kujikimu pekee na wana mchango mdogo kwenye uchumi.**[44]**

Jambo la kuzingatiwa kuhusu usalama wa chakula lingezingatia namna nyingine za uzalishaji chakula,mfano ulimaji mazao *ukusiphilisa*

(‘kwaajili ya kujikimu’). Sanjari na hii, dhana ya uhuru wa chakula ilizaliwa miaka ya 1990 kuchagiza suala la ‘haki ya watu kwa chakula bora na chakula kinachozalishwa kwa kukidhi msingi wa kitamaduni kupitia njia endelevu na haki za kuamua mifumo yao ya chakula na kilimo’.**[45]** Kuweka kipaumbele kwa uhuru wa chakula kama njia mbadala ya kuratibu mfumo wetu wa chakula unaowapa kauli wale wenye kuifanyia kazi ardhi juu ya namna ya kuratibu sekta ya kilimo na vipi vyapaswa kuwa vipaumbele vyenye tija.

Hata hivyo,uhuru wa chakula na *ukusiphilisa* – sambamba na mahusiano baina ya wafanyakazi wa mashambani na ardhi-yanapuuzwa na suluhu za kibepari za uzalishaji chakula.

Hamasa ya ardhi kwa wafanyakazi wa mashambani ni kubwa kushinda malengo kuzalisha chakula chao na familia zao;wanajitizama wao kama wakulima, kama hasa wenye kuifanyia kazi ardhi,kama wazalishaji wa chakula na wafugaji wa mifugo, na wanaamini juu ya uwezo wao katika kuchangia uendelevu kwa masoko ya ndani na bara zima. Programu madhubuti mpya ya ugawanyaji ni lazima iunge mkono matamanio yao.



Sbongile Tabhethe akifanya kazi katika bustani ya chakula huko eKhenana, makaazi yanayosaidiwa na vuguvugu la watu wa makaazi duni la Abahlali baseMjondolo  huko Cato Manor,Durban, tarehe 9 Juni 2020.

Hisani: New Frame / Mlungisi Mbele

## *Majumuisho*

Mageuzi ya ardhi nchini Afrika kusini yameshindwa kabisa kuleta suluhu dhidi ya ukatili wa ukoloni na ubaguzi wa rangi. Serikali za baada ya kipindi cha ubaguzi wa rangi(apartheid) zilichukua uelekeo wa soko

katika suala la mgawanyo wa ardhi kwa kutoa kipaumbele kwa ‘ mfumo wa hiyari ya mnunuzi,hiyari ya muuzaji’, ambayo iliongeza zaidi hali ya kutokuwepo usawa. Wanufaika wakubwa wa ardhi hata sasa ni ni watu wachache wa tabaka la juu  na makampuni ya kilimo ambayo yanakopesheka katika taasisi za fedha. Mageuzi ya ardhi kama yalivyo hayajarejesha haki  wala kutatua tatizo la njaa ya ardhi miongoni mwa wafanyakazi wa mashambani wengi weusi  ambao wamezalisha utajiri kwa wamiliki wa mashamba kwa vizazi na vizazi.

Suala la mgawanyo wa ardhi ni la haraka kwaajili ya kutibu ‘maovu ya kihistoria’ na kusuluhisha hali ya sasa ya kutokuwepo usawa wa kiuchumi na kijamii ili kupata mustakabali usawa kwa wote.**[46]** Hivi sasa nchini Afrika Kusini,wafanyakazi wa mashambani wanaishi mazingira yanayowaondolea utu wao.Majimbo yote tisa ya nchi ya nchi yanakabiliwa na tatizo la kuwaondoa watu kwenye maeneo yao ya makaazi na uzalishaji(eviction) licha ya kuwepo kwa sheria zinazotakiwa kuzuia watu kuondolewa mfano sheria ya Ulinzi wa Ardhi namba 62 ya mwaka 1997(Extension of Security of Tenure Act 62 of 1997). Katika nyakati ambapo wakaazi wa mashambani walikabiliana na mazoezi ya kuwaondoa, wamiliki wa  mashamba hukata huduma za msingi kama vile umeme na maji kama mbinu za kuwashinikizakuondoka katika mashamba.Mazingira ya kazi na ya kuishi katika mashamba ni mabaya,na watu wanaoishi na kufanya kazi mule hawapati huduma bora za elimu na afya, hali inayoendelea kuwafunga katika lindi la umasikini.

Vizazi vya wafanyakazi waliosahaulika kwa karne nyingi zilizopita wanadai fidia. Mjadala wa mgawanyo-mpya wa ardhi ambao kwa makusudi unapuuza namna ya kiafrika ya mahusiano na ardhi unaendeleza mradi wa ukoloni na unashikilia kutweza utu.Programu yeyote ya mgawanyo-mpya wa ardhi itakayopuuza madai haya basi haikidhi.

Madai yafuatayo kutoka kwa wafanyakazi na wakaazi wa mashambani ni kijenzi muhimu na madhubuti kwa programu ya mageuzi ya ardhi:

1. Serikali ya Afrika Kusini lazima ikutane na wafanyakazi wa na wakaazi wa mashambani ili kuchukua na kuingiza michango na uzoefu wao katika uundaji wa programu ya mageuzi ya ardhi inayoelezea mahitaji yao ya ardhi.
2. Madai ya wafanyakazi wa kupangishwa kuhusu ardhi lazima yapewe kipaumbele ili kuepusha mageuzi ya ardhi yatakayowatajirisha watu weusi wachache.
3. Idara ya Kilimo,Mageuzi ya Ardhi na Maendeleo Vijijini isimamie mchakato wa kupunguza na kugawanya kwa sehemu ardhi za wamiliki wa kizungu kwa waajiriwa wa kudumu na vizazi vya wafanyakazi wa mashambani ambao wamefanya kazi katika mashamba husika kwa vizazi kadhaa.

4. Serikali  lazima inunue mashamba kwaajili ya wafanyakazi wa mashambani na kuwasaidia  kwa mitaji ya awali ,pembejeo na stadi za kilimo.
5. Mageuzi ya ardhi nchini Afrika Kusini  lazima yazingatie masuala ya kijamii yanayopelekea uhaba wa chakula na kuzitambua fursa zilizopo kufanya marekebisho kupitia mgawanyo mpya wa ardhi.
6. Mchakato wa mageuzi ya ardhi lazima  uzingatie hali ya manyanyaso ya wanawake maeneo ya kazi katika sekta ya kilimo na ukosemu wa haki za umiliki ardhi kwa wanawake wakulima ili kuondoa pengo la kijinsia katika maeneo yote.

*Loo ngumhlaba wookhokho bethu!* Ardhi hii ni ya wazee wetu! Ni wasaa muafaka kwa wanaoizalisha kupata haki ya umiliki wa ardhi.

## *Bibliography*

**Adams, Martin, Sipho Sibanda, and Stephen Turner**. 'Land Tenure Reform and Rural Livelihoods in Southern Africa'. *Natural Resource Perspectives*, no. 39 (February 1999): 1–15.

**Amanor, Kojo S.** 'Land Governance in Africa: How Historical Context Has Shaped Key Contemporary Issues Relating to Policy on Land'. In

*Framing the Debate Series*, no. 1. Rome: International Land Coalition, 2012.

**Association for Rural Advancement (AFRA).** *The Investigation of the Effects of Conservation and Tourism on Land Tenure and Ownership Patterns in KwaZulu-Natal*. Pietermaritzburg: AFRA, 2004.

**Atkinson, Doreen.** *Going for Broke: The Fate of Farm Workers in Arid South Africa*. Cape Town: Human Sciences Research Council Press, 2007.

**Bab'Kubheka.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Newcastle, KwaZulu-Natal, 23 October 2021.

**Bhut'Ben.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Mooi River, KwaZulu-Natal, 24 October 2021.

**Bhattacharya, Tithi.** 'Mapping Social Reproduction Theory'. *Verso Books Blog*, 15 February 2018. **https://www.versobooks.com/blogs/3555-mapping-social-reproduction-theory**.

**Baucom, Ian.** 'Specters of the Atlantic'. *The South Atlantic Quarterly* 100, no. 1 (2001): 61–82.

**Baw'uMkwayi.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Nyarha, Eastern Cape, 5 June 2021.

**Baw'uSukwini.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Nyarha, Eastern Cape, 5 June 2021.

**Carmen Louw.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Stellenbosch, Western Cape 14 March 2022.

**Credit Suisse Research Institute.** *Global Wealth Report 2021*. June 2021. **https://www.credit-suisse.com/about-us/en/reports-research/global-wealth-report.html**.

**Cross, Catherine and Michelle Friedman.** 'Women and Tenure: Marginality and the Left-hand Power'. In *Women, Land, and Authority: Perspectives from South Africa*, edited by Shamim Meer, 17–34. Cape Town: David Philip, 1997.

**Davies, Wendy.** *We Cry for Our Land: Farm Workers in South Africa*. Oxford: Oxfam, 1990.

**Department of Rural Development and Land Reform, Republic of South Africa.** *Land Audit Report, Version 2: Private Land Ownership by Race, Gender, and Nationality*. Department of Rural Development and Land Reform, November 2017.

**Devereux, Stephen, Ruth Hall, and Colette Solomon.** 'The Farm Workers Who Produce Our Food Are the Most Vulnerable to Hunger'. *Mail & Guardian*, 8 October 2019. **https://mg.co.za/article/2019-10-08-00-the-farm-workers-who-produce-our-food-are-the-most-vulnerable-to-hunger/**.

**Du Toit, Andries.** 'Farm Workers and the "Agrarian Question"'. *Review of African Political Economy* 21, no. 61 (1994): 375–388.

**Food and Agriculture Organisation of the United Nations (FAO), International Fund for Agricultural Development, United Nations International Children's Emergency Fund, World Food Programme, and World Health Organisation**. *The State of Food Security and Nutrition in the World 2021: Transforming Food Systems for Food Security, Improved Nutrition, and Affordable Healthy Diets for All*. Rome: FAO, 2021.

**Food and Agriculture Organisation of the United Nations.** 'Food Security'. *Policy Brief*, no. 2 (2006): 1–4.

Hornby, Donna and Stha Yeni. 'Farm Dwellers in Kwa-Zulu Natal South Africa and the Politics of Home'. Conference Paper no. 74 presented at the Emancipatory Rural Politics Initiative Conference, 2018.

**Karanja, Perpetua W.** 'Women's Land Ownership Rights in Kenya'. *Third World Legal Studies* 10, article 6 (1991): 109–135.

**Leana, Tanie**. Interview and translation by Yvonne Phyllis. Colesberg, Northern Cape, 6 February 2022.

**London, Leslie.** 'The "Dop" System, Alcohol Abuse, and Social Control Amongst Farm Workers in South Africa: A Public Health Challenge'. *Social Science & Medicine* 48, no. 10 (1999): 1407–1414.

**Mafeje, Archibald B.** *The Agrarian Question, Access to Land, and Peasant Responses in sub-Saharan Africa*. Geneva: United Nations Research Institute for Social Development, 2003.

**MamNteshi.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Newcastle, KwaZulu-Natal, 23 October 2021.

**MaNkomo.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Mooi River, KwaZulu-Natal, 24 October 2021.

**MamNywabe.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Nyarha, Eastern Cape, 6 June 2021.

**Mkhize, Naledi N.** 'Private Game Farms and the Tenure Security of Workers and Dwellers in Cradock – Implications for Tenure Reform in South Africa'. PhD diss., University of Cape, 2012.

**Moore, Melissa.** 'SA's Agriculture Sector – A Key Driver of Economic Growth'. *Future Growth*, 31 May 2021.

**https://www.futuregrowth.co.za/insights/sa-s-agriculture-sector-a-key-driver-of-economic-growth/**.

**Moyo, Sam.** 'The Politics of Land Distribution and Race Relations in Southern Africa'. Identities, Conflict, and Cohesion Programme Paper no. 10, United Nations Research Institute for Social Development, 2004.

**Neocosmos, Michael.** *The Agrarian Question in Africa and the Concept of 'Accumulation from Below': Economics and Politics in the Struggle for Democracy* (*Research Report)*. Vol. 93. Nordic Africa Institute, 1993.

**Ngcukaitobi, Tembeka.** 'Part Two: Land Matters and Historical Distortions'. Interview by Yvonne Phyllis. *New Frame*, 7 July 2021. **https://www.newframe.com/part-two-land-matters-and-historical-distortions/**.

**Ngcukaitobi**, **Tembeka.** 'Rethinking the Past and Future of Land Reform'. *New Frame*, 19 November 2019. **https://www.newframe.com/rethinking-the-past-and-future-of-land-reform/**.

**Oom Boetman.** Interview by Yvonne Phyllis. Colesburg, Northern Cape, 6 February 2022.

**Ossome, Lyn and Sirisha C. Naidu.** 'Social Reproduction and the Agrarian Question of Women's Labour in India'. *Agrarian South: Journal of Political Economy* 5, no. 1 (2016): 50–76.

**Ossome, Lyn.** 'Episode 8: Social Reproduction, Capitalist Exploitation and Surplus the Population'. 15 October 2021, in *Institute for Poverty, Land and Agrarian Studies (PLAAS) Podcast*, audio, 39:35. **https://www.plaas.org.za/podcast-social-reproduction-capitalist-exploitation-and-the-surplus-population-2/**.

**Ossome, Lyn, and Sirisha C. Naidu.** 'The Agrarian Question of Gendered Labour'. In *Labour Questions in the Global South*, edited by Praveen Jha, Walter Chambati, and Lyn Ossome, 63–86. Singapore: Palgrave Macmillan, 2021.

**Patel, Raj.** 'Climate, Conflict and Capitalism Drive Global Hunger. COVID Made It Worse'. *Democracy Now*, 23 September 2021. **https://www.democracynow.org/2021/9/23/raj_patel_un_food_systems_summit**.

**Rodney, Walter.** *How Europe Underdeveloped Africa*. London: Verso Books, 2018.

**Ryno Filander.** Interview and translation by Yvonne Phyllis. Bellville, Western Cape, 26 July 2021.

**Shivji, Issa G.** *Accumulation in an African Periphery: A Theoretical Framework*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers, 2009.

**Shivji, Issa G.** 'Commodification of the Commons in the Transition to Neo-Liberalism: The Case of Tanzania'. Online lecture in The Political Economy of Land Governance in Africa seminars, Network of Excellence for Land Governance in Africa, 9 September 2021.

**Shivji**, **Issa G.** 'Let a Hundred Socialist Flowers Bloom: A Conversation with Issa Shivji'. Interview by Freedom Mazwi. *Review of African Political Economy*, 11 November 2021. **https://roape.net/2021/11/11/let-a-hundred-socialist-flowers-bloom-a-conversation-with-issa-shivji/.**

**Shivji, Issa G.** 'Sam Moyo and Samir Amin on the Peasant Question'. *Agrarian South: Journal of Political Economy* 8, no. 1–2 (2019): 287–302.

**Shivji, Issa G**. 'Trajectories of Accumulation: How Neoliberal Primitive Accumulation is Planting the Seeds of Suicide'. *New Agenda: South African Journal of Social and Economic Policy*, no. 68 (2018): 36–38.

**Skosana, Dineo.** 'Grave Matters: The Contentious Politics of Gravesite Removals in Contemporary South Africa – The Case of Tweefontein, Ogies'. PhD diss., University of Witwatersrand, 2019.

**Skosana**, **Dineo**. 'Mining Activities Continue to Dispossess Black Families in South Africa'. *Bizcommunity*, 12 November 2019. **https://www.bizcommunity.com/Article/196/608/197777.html**.

**Statistics South Africa**. 'Stats SA Releases Census of Commercial Agriculture 2017 Report'. *Stats SA*, 24 March 2020. **http://www.statssa.gov.za/?p=13144**.

## Endnotes

[1] This dossier is written in the first person by the author, Yvonne Phyllis, a descendant of farmworkers. The use of the first person has been retained to reflect the intimate nature of politics surrounding the issue of land in South Africa.

**[2]** Andries du Toit, 'Farm Workers and the "Agrarian Question"', *Review of African Political Economy*, no. 61 (1994): 375.

**[3]** Tithi Bhattacharya, 'Mapping Social Reproduction Theory', Verso Books Blog, 15 February 2018, **https://www.versobooks.com/blogs/3555-mapping-social-reproduction-theory**.

**[4]** Bab'Kubheka speaks in plural when referring to fathers, forefathers, or ancestors because he understands his family's struggles to be part of

the class struggle of all Black farmworkers, farm dwellers, and labour tenants. This way of speaking is common in many African cultures.

**[5]** Bab'Kubheka, interview and translation by Yvonne Phyllis, Newcastle, KwaZulu-Natal, 23 October 2021.

**[6]** Walter Rodney, *How Europe Underdeveloped Africa* (London: Verso Books, 2018), 271.

**[7]** For more on this topic, see Tembeka Ngcukaitobi, 'Part Two: Land Matters and Historical Distortions', interviewed by Yvonne Phyllis, *New Frame*, 7 July 2021.

**[8]** Ian Baucom, 'Specters of the Atlantic', *The South Atlantic Quarterly* 100, no. 1 (2001): 61–82.

**[9]** Wendy Davis, *We Cry for Our Land: Farm Workers in South Africa* (London: Oxfam, 1990), 1.

**[10]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[11]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[12]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[13]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[14]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[15]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[16]** Davies, *We Cry for Our Land*, 1.

**[17]** Issa G. Shivji, 'Trajectories of Accumulation: How Neoliberal Primitive Accumulation is Planting the Seeds of Suicide', *New Agenda: South African Journal of Social and Economic Policy*, no. 68 (2018): 36.

**[18]** Credit Suisse Research Institute, *Global Wealth Report 2021*.

**[19]** Statistics South Africa, 'Stats SA Releases Census of Commercial Agriculture 2017 Report,' *Stats SA*, 24 March 2020, **http://www.statssa.gov.za/?p=13144**.

**[20]** Department of Rural Development and Land Reform, Republic of South Africa, *Land Audit Report, Version 2: Private Land Ownership by Race, Gender, and Nationality*, Department of Rural Development and Land Reform, November 2017.

**[21]** In the 1950s, the apartheid government divided South Africans into four racial groups: white, native (or Black), Indian, and Coloured (mixed-race people).

These racial and cultural descriptors are no longer legislated as they were during the apartheid years but are still in common use today. For more on race and ethnicity in South Africa, see South African History Online,

‘Race and Ethnicity in South Africa’, 27 August 2019, **https://www.sahistory.org.za/article/race-and-ethnicity-south-africa**.

**[22]** Perpetua Wambui Karanja, ‘Women’s Land Ownership Rights in Kenya’, *Third World Legal Studies* 10, article 6 (1991): 109.

**[23]** MamNywabe, interview and translation by Yvonne Phyllis, Nyarha, Eastern Cape, 6 June 2021.

**[24]** Issa G. Shivji, *Accumulation in an African Periphery: A Theoretical Framework* (Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers, 2009), 26.

**[25]** Issa G. Shivji, ‘Commodification of the Commons in the Transition to Neo-Liberalism: The Case of Tanzania’, (Online lecture in The Political Economy of Land Governance in Africa seminars, Network of Excellence for Land Governance in Africa, 9 September 2021).

**[26]** Shivji, ‘Commodification of the Commons in the Transition to Neo-Liberalism’, 2021.

**[27]** Credit Suisse Research Institute, *Global Wealth Report 2021*.

**[28]** Carmen Louw, interview and translation by Yvonne Phyllis, Stellenbosch, Western Cape, 14 March 2022.

**[29]** Moyo, ‘The politics of land distribution’, 2.

**[30]** Oom Boetman, interview by Yvonne Phyllis, Colesberg, Northern Cape, 6 February 2022.

**[31]** Tanie Leana, interview and translation by Yvonne Phyllis, Colesberg, Northern Cape, 6 February 2022.

**[32]** Baw'uSukwini, interview and translation by Yvonne Phyllis, Nyarha, Eastern Cape, 5 June 2021.

**[33]** Baw'uMkwayi, interview and translation by Yvonne Phyllis, Nyarha, Eastern Cape, 5 June 2021.

**[34]** Ryno Filander, interview by Yvonne Phyllis, Bellville, Western Cape, 26 July 2021.

**[35]** Leslie London, 'The "Dop" System, Alcohol Abuse and Social Control Amongst Farmworkers in South Africa: A Public Health Challenge', *Social Science & Medicine* 48, no. 10 (1999): 1407–1414.

**[36]** MaNkomo, interview and translation by Yvonne Phyllis, Mooi River, KwaZulu-Natal, 24 October 2021.

**[37]** Dineo Skosana, 'Mining Activities Continue to Dispossess Black Families in South Africa', *Bizcommunity*, 12 November 2019, **https://www.bizcommunity.com/Article/196/608/197777.html**.

**[38]** Dineo Skosana, 'Grave Matters: The Contentious Politics of Gravesite Removals in Contemporary South Africa – The Case of Tweefontein, Ogies', (PhD diss., University of Witwatersrand, 2019).

**[39]** Bhut'Ben, interview and translation by Yvonne Phyllis, Mooi River, KwaZulu-Natal, 24 October 2021.

**[40]** FAO, International Fund for Agricultural Development, United Nations International Children's Emergency Fund, World Food Programme and World Health Organisation, *The State of Food Security and Nutrition in the World 2021*, 2021.

**[41]** FAO, *The State of Food Security and Nutrition in the World 2021*, 2021.

**[42]** Stephen Devereux, Ruth Hall, and Colette Solomon, 'The Farm Workers Who Produce Our Food Are the Most Vulnerable to Hunger', *Mail & Guardian*, 8 October 2019, **https://mg.co.za/article/2019-10-08-00-the-farm-workers-who-produce-our-food-are-the-most-vulnerable-to-hunger/.**

**[43]** Review of African Political Economy (ROAPE), 'Let a Hundred Socialist Flowers Bloom: A Conversation with Issa Shivji', *ROAPE*, 11 November 2021, **https://roape.net/2021/11/11/let-a-hundred-socialist-flowers-bloom-a-conversation-with-issa-shivji/.**

**[44]** Moyo, 'The Politics of Land Distribution', 2.

**[45]** Tricontinental: Institute for Social Research, '*A World Without Hunger: The Fortieth Newsletter (2021)*', October 2021, https://thetricontinental.org/newsletterissue/40-a-world-without-hunger/.

**[46]** Tembeka Ngcukaitobi, 'Rethinking the Past and Future of Land Reform', *New Frame*, 19 November 2019, **https://www.newframe.com/rethinking-the-past-and-future-of-land-reform/**.